
UmeBima 3.0_Afya Salama.pdf 1 02/03/2023 08:41



# MPANGO WA BIMA YA AFYA YA **AFYA SALAMA**

**UTANGULIZI**

Huu ni mpango maalumu wa bima nafuu ya afya kwa ajili ya watu binafsi, familia na vikundi mbalimbali

**FAIDA ZA MPANGO HUU NI ZIPI?**

Mpango huu unatoa mafao yaliyotajwa hapo chini. Mafao hayo yatatolewa kwa kuzingatia sheria na masharti ya mpango huu. MAFAO YOTE NI KWA FAMILIA NZIMA KWA MWAKA.

| MAFAO YALIYOMO KATIKA MPANGO WA BIMA YA AFYA SALAMA | |
|---|---|
| **UKOMO WA MAFAO YA KULAZWA inagharamia matibabu yote ya kulazwa hospitalini baada tu ya kupata idhini ya awali** | |
| Mwanachama peke yake | TZS 2,000,000 |
| Mwanachama na mtegemezi mmoja | TZS 2,500,000 |
| Mwanachama na wategemezi wawili | TZS 2,750,000 |
| Mwanachama na wategemezi watatu au zaidi | TZS 3,000,000 |
| Wodi ya jumla/wengi kwa matibabu ya kulazwa | Imejumuishwa |
| ICU & ICCU | Imejumuishwa |
| Chumba cha upasuaji, oparesheni, madawa, vifaa tiba, huduma za damu & kusafisha/kufunga vidonda | Imejumuishwa |
| Kumuona daktari & Matibabu | Imejumuishwa |
| Tiba za mionzi zikiwemo X-Ray, Ultrasound, CT Scan, MRI & Bone Densitometry scan (ukomo wa malipo kwa matibabu haya ni TZS 500,000) | Imejumuishwa |
| Vipimo vya Maabara kwa mwanachama aliyelazwa | Imejumuishwa |
| Mazoezi tiba kwa mgonjwa aliyelazwa | Imejumuishwa |
| Uzazi (kliniki ya wajawazito, wodi, kujifungua kwa kawaida au oparesheni, na matatizo mengine yatakayotokana na ujauzito, kabla, wakati na baada ya kujifungua). Ukomo wa malipo kwa matibabu hay ani TZS 600,000. | Imejumuishwa |
| Oparesheni za usoni, mifupa ya usoni na mdomoni kwa matatizo ya kansa na ajali | Imejumuishwa |
| Matibabu ya kansa | Imejumuishwa |
| Magonjwa Sugu au ya muda mrefu na magonjwa nyemelezi yanayohusiana na maambukizi ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi | Imejumuishwa |
| **MAFAO YA MAGONJWA YA NJE (Ndani ya Tanzania tu)** | |
| Kumuona mganga & mganga mbobezi | Imejumuishwa |
| X-Ray | Imejumuishwa |
| Vipimo vya maabara | Imejumuishwa |
| Majeraha na dharura | Imejumuishwa |
| Madawa ya magonjwa ya muda mfupi na mrefu | Imejumuishwa |
| **Ukomo wa mafao ya magonjwa ya nje kwa Mwanachama/Familia** | |
| Mwanachama peke yake | TZS 300,000 |
| Mwanachama na mtegemezi mmoja | TZS 350,000 |
| Mwanachama na wategemezi wawili | TZS 400,000 |
| Mwanachama na wategemezi wa tatu na zaidi | TZS 450,000 |

**N.B.**
ICU – Kitengo cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu/mahututi
ICCU – Kitengo cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu wa moyo.

| JEDWALI LA MALIPO: | |
|---|---|
| **MALIPO YA MWAKA YA BIMA KWA FAMILIA** | |
| Mwanachama pekee hadi familia ya watu wanne (M+3) | TZS 200,000 |
| Mwanachama yeyote atakayeongezeka | TZS 80,000 |

**ANGALIZO:**

Kutakuwa na ukomo wa matibabu ya nje kwa siku kwa mwanachama hadi TZS 60,000

**SIFA ZA ANAYESTAHILI KUJIUNGA NA MPANGO HUU WA BIMA**

- Umri wa juu wa kujiunga ni miaka 70
- Ukubwa wa familia ni Mwanachama na wategemezi watano. Hii inajumuisha Mwanachama mchangiaji, mwenza wa ndoa na Watoto wake wa kuwazaa wanne wenye umri chini ya miaka hadi 18. Mpango huu utajumuisha pia mtoto tegemezi mwenye umri chini ya miaka 21 ambaye hajaoa/kuolewa na bado ni mwanafunzi katika chuo/taasisi inayotambuliwa na Serikali
- Mwanachama ataruhusiwa kupata huduma kupitia vituo vya Afya/ Hospitali na Maduka ya Dawa yaliyoorodheshwa.

**KIPINDI CHA KUSUBIRIA**

- Miezi tisa ya kusubiria kwa matibabu yote yanayohusiana na Uzazi
- Miezi kumi na mbili ya kusubiria kwa Matibabu ya kulazwa ya muda mrefu na magonjwa ambayo mwanachama/mtegemezi alikuwa nayo kabla ya kujiunga na bima

**HUDUMA AMBAZO HAZIPO KATIKA BIMA HII**

**Huduma zifuatazo hazitakuwa sehemu ya bima hii**

- Gharama zilizokwisha lipwa na bima nyingine kwa tatizo/ugonjwa huo huo
- Magonjwa/matatizo ya meno na macho isipokuwa yale yanayotokana na ajali
- Matibabu yaliyofanyika kwa mtoa huduma asiyekuwa na mkataba na Strategis Insurance (T) Limited.
- Matibabu/upasuaji wowote ule uliofanyika kwa ajili ya urembo ama upasuaji wa plastiki
- Uzazi wa mpango na matibabu ya utasa
- Matibabu ya mwanachama kulipa fedha taslimu kwa mtoa huduma kwa lengo la kuja kuomba kurudishiwa fedha.

Rejea karatasi ya mpango kwa idadi kamili ya matibabu/vifaa/huduma zisizokuwemo kwenye mpango hu una mengineyo.

Strategis Insurance Tanzania Limited.